


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI



**TANGAZO LA NAFASI MBILI (2) ZA UJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uteuzi (**Nomination Committee**) iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Na. 12 ya mwaka 2003 anawakaribisha Watanzania wenye sifa stahiki zinazofafanuliwa kwenye Tangazo hili, kuomba kuteuliwa kujaza nafasi mbili zilizo wazi katika Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA. Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia matakwa ya Vifungu vya 7(5) na 11 vya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya mwaka 2003 na kutokuwa na maslahi kinzani (**Conflict of Interests**) na majukumu ya TCRA.

Wasifu stahiki wa Waombaji

Kwa mujibu wa Jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, anayeweza kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA anapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Awe mwenye Shahada kutoka Chuo Kikuu kinachotambuliwa;
- (ii) Awe mwenye uzoefu kazini kwa walao miaka kumi (10) katika moja au zaidi ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Uchumi, Fedha, Uhandisi, Utangazaji au Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;
- (iii) Awe mwenye ufahamu wa Sekta;
- (iv) Airidhishe Kamati ya Uteuzi kuwa hana, na hatarajiwi kuwa na maslahi kinzani inavyoainishwa katika Kifungu cha 11 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania;
- (v) Awe mwenye hiari na utayari wa kuhudumu kama Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania;
- (vi) Kwa maoni ya Kamati ya Uteuzi, awe anayefaa kutekeleza kwa weledi na uaminifu majukumu na wajibu za Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.


*Waombaji wenye uzoefu (waliobobea) katika fani za **Utangazaji** na **TEHAMA** watapewa kipaumbele.*

Maombi yote yakiwa yameambatishwa na Wasifu Binafsi (**Curriculum Vitae - CV**) wa mwombaji na majina na anuani za Wadhamini watatu (3), mmojawapo akiwa ni Mwajiri wa mwisho au wa sasa (**the last or current Employer**), yatumwe kwa: -

Mwenyekiti,
Kamati ya Uteuzi ya Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,
Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ujenzi,
S.L.P 677

40470 DODOMA.

Maombi yawasilishwe kwa Mwenyekiti kabla, au ifikapo tarehe 25 Juni, 2021


Dkt. Zainab A. S. Chaula

MWENYEKITI WA KAMATI YA UTEUZI BODI YA TCRA